1:1-22 MIAKA KUMI YA TAABU KATIKA NCHI YA MOABU

Njaa kali ilipoleta shida kubwa katika Israeli, Alimeleki aliwachukua mke wake Naomi na wanawe wawili akavuka Yordani na kuishi katika nchi ya Moabu, akitumaini kwamba huko angeweza kuishi bila taabu zaidi. Lakini Alimeleki alikufa, na katika muda wa miaka kumi wanawe wawili ambao walikuwa wameoa wanawake wa Kimoabu, walikufa vile vile (1:1-5).

Naomi hakuona matumaini yo yote ya maisha mazuri huko Moabu. Kwa hiyo, aliposikia kwamba njaa kali ya Israeli ilikwisha, aliamua kurudi nyumbani. Wakwe zake wawili waliompenda sana, waliamua kufuatana naye na kumsaidia katika kazi yake (6-10).

Naomi pia aliwapenda wanawake wale, na kwa kuwa wote wawili hawakuwa na watoto, wangekuwa na hali hiyo daima kama wangeishi naye, kwa sababu Naomi hakuwa na wana wengine ambao wangeweza kuwaoa. (Mila yao ilidai kwamba iwapo mwanamme anakufa bila kuwa na watoto, ndugu yake am woe mjane wake kwa muda mpaka wanapopata mtoto. Mtoto huyo ahesabiwe kuwa ni wa ndugu aliyekufa, naye arithi jina lake na baadaye arithi mali yake; taz.Kum 25:5-10; Mk 12:19.) Kwa hiyo Naomi aliwaeleza wazi kwamba wasingekuwa na haja yo yote ya kufuatana naye. Wawe hum kabisa kubaki na watu wao na kuanza maisha mapya kwa njia ya kuolewa upya na kupata nyumba zao wenyewe (11-13).

Mkwe mmoja alikubali ushauri wa Naomi akawarudia watu wake wa Moabu. Lakini mwingine, Ruthu, aliamua kufuatana na Naomi na kumtumaini Mungu wake kwa hali yo yote (14-18). Ingawa Naomi alikaribishwa nyumbani na watu wa mji wake, alisikitika sana alipofikiri mambo yote aliyoyakosa katika muda wote wa miaka kumi iliyopita (19-22).

2:1-4:22 MWANZO MPYA KATIKA ISRAELI

Ruthu afanya kazi katika shamba la Boazi (2:1-23)

Huko Israeli haikuchukua muda mrefu kueleweka kwamba Mungu alikuwa ameyatawala mambo ya maisha ya wajane wale wawili. Kufuatana na sheria ya Israeli, mkulima aliyevuna mashamba yake hakutakiwa kuwatuma watu wake shambani mara ya pili, ili waokote nafaka zilizosalia au zilizoanguka nyuma ya wavunaji. Masazo hayo yalitakiwa yaachwe kwa ajili ya maskini ambao wangewafuata wavunaji na kuokota kilichobaki (Law 23:22; Kum 24:19). Kwa hiyo Ruthu alikwenda kuokota masazo, ili yeye na Naomi wapate chakula kidogo. Ruthu hakujua kwamba, kwa bahati shamba lile alipookota masazo lilikuwa mali ya jamaa wa marehemu mkwewe. Jina la mtu yule lilikuwa Boazi (2:1-7).

Boazi alikuwa amesikia habari za wema ambao Ruthu alimfanyia mkwewe Naomi, kwa hiyo alimpa thawabu kwa njia ya kumkaribisha chakula na maji, kwa kumlinda asisumbuliwe na vijana wa mahali pale na kwa kuwaambia wavunaji wamwachie masuke ya kutosha, ili aweze kuyaokota (8-16).

Kutokana na wema wa Boazi na bidii yake mwenyewe, Ruthu alipata chakula kingi kuliko alivyokuwa akitazamia. Naomi aliposikia habari yake, alijua kwamba Mungu aliongoza mambo vizuri. Alimwambia Ruthu kwamba mtu yule aliyemwonyesha wema alikuwa jamaa wa karibu wa marehemu mume wake (17-20). Ruthu aliendelea kuokota masazo katika shamba la Boazi mpaka mwisho wa msimu (21-23).

Mpango wa Naomi (3:1-18)

Mavuno yalipomalizika, wajane wawili walipata nafaka za kutosha mpaka msimu wa mavuno ya muhula. Lakini Naomi alifikiri juu ya maisha ya Ruthu akatoa ushauri kwamba aolewe tena (3:1).

Tatizo moja lilikuwa kwamba hawakubaki wana hai wa Naomi, maana yake hawakuwepo ndugu zake marehemu mumewe Ruthu ambao wangeweza kumwoa Ruthu. Kwa hiyo Naomi alimfikiria Boazi, kwa sababu alimwona yeye kuwa jamaa wa karibu. Zaidi ya hayo, Boazi alikuwa ameonyesha kwamba hakumchukia Ruthu. Hivyo Naomi alizingatia mpango ambao Ruthu angeweza kuongea na Boazi kwa utulivu bila watu wengine kupata habari. Ikawa usiku mmoja Ruthu akaenda mahali pa kupepetea nafaka ambapo Boazi alilala ili kulinda nafaka yake. Kwa uangalifu sana alifunua blanketi miguuni pake, ili kutokana na baridi Boazi aamke pole pole. Kisha, wakati watu wengine walipolala usingizi, Ruthu alimweleza habari zake. Kwa kumwomba Boazi 'amfunike Ruthu nguo yake', alimwomba kwa njia ya fumbo amchukue kuwa mke wake (2-9).

Boazi alifurahi sana kuheshimiwa namna hiyo. Alijua kwamba ingalikuwa rahisi sana kwa Ruthu kuolewa na wanaume wa mahali pale ambao wangelingana naye zaidi kwa umri kuliko yeye. Lakini

Ruthu alitaka kuwa mwaminifu kwa wajibu wa ukoo wake. Kwa hiyo Boazi naye alimwonyesha uaminifu wake, akimwambia Ruthu kwamba alikuwepo jamaa wa karibu zaidi kuliko yeye ambaye angekuwa na haki ya kumwoa. Ila kama yule jamaa asingetaka, Boazi angemchukua kuwa mkewe (10-13).

Ruthu alibaki katika uwanja wa kupiga nafaka kwa muda. Kisha Boazi alimpa nafaka zaidi na kumtuma nyumbani kabla ya mapambazuko, kwa sababu hakutaka watu wamwone na kuanzisha uzushi (14-15). Naomi alifurahi kuona mambo yalikwenda alivyotumaini (16-18).

Boazi amwoa Ruthu (4:1-22)

Naomi aliyeona taabu ya ujane wake, aliamua kuuza mashamba ya marehemu mume wake. Ili kuzuia urithi huo usiende nje ya ukoo wake, ilimbidi kuhakikisha kwamba mashamba hayo yananunuliwa (yaani kukombolewa) na jamaa wa karibu sana (taz.Law 25:23-28). Mtu aliyehusika hapo alikuwa yule yule ambaye angepaswa pia kumchukua Ruthu na kuzaa naye mrithi ambaye angechukua jina la marehemu Elimeleki (mumewe Naomi) na la Maloni (mwanawe Elimeleki na mumewe Ruthu). Lakini kama mrithi huyo angezaliwa, angerithi mali ya ukoo wake. Maana yake ingekuwa kwamba, yule jamaa ambaye angenunua mali ya Naomi, baadaye mali hiyo ingempotea tena, kama angemzaa mwana na Ruthu. Jamaa yule alikuwa tayari kununua mashamba ya Naomi, lakini kumwoa Ruthu ingekuwa hasara kwake, na hivyo alikataa (4:1-6).

Kwa njia ya sherehe ya kuvua kiatu chake na kumpa Boazi, mtu yule aliyekuwa na haki ya kununua mali ya Naomi, alionyesha kwamba haki yake alimkabidhi Boazi. Wakati huo njia ilikuwa wazi kwa Boazi kumwoa Ruthu. Jambo hili pia lilimpa Boazi nafasi ya kulihifadhi jina la ukoo wa Elimeleki (na la Maloni), kuhifadhi mali ya ukoo wa Elimeleki, na vile vile kumwoa mwanamke aliyempenda (7-10). Mashahidi walioona sherehe hiyo waliwapa pongezi Boazi na Ruthu, wakiwatakia kwamba Mungu awafanikishe wazao wao, kama alivyowafanikisha na kuwabariki mababu wa Israeli (11-12).

Mtoto aliyezaliwa na Boazi na Ruthu alimfurahisha Naomi, lakini baraka zaidi katika maisha yake ilikuwa upendo alioonyeshwa na binti mkwe, Ruthu (13-15).Katika historia ya baadaye dua lile la mashahidi wa mashauri ya Boazi na Ruthu lilitimizwa kwa kiasi kikubwa sana ambavyo hata wale walioliombea wasingeweza kuhisi. Mtoto aliyezaliwa nao, licha ya kuchukua jina na urithi wa mumewe Naomi, alikuwa babu wa mfalme Daudi (Obedi), na mzazi mmojawao wa Yesu aliye Masihi (13-22; taz.Mt 1:1,5).